ALHAMISI APRILI 27- MEI 3, 2023

# Ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa

Inatoka Uk. 9

ndama.

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupata maziwa pungufu na kumdhoofisha ndama na ng'ombe.

Kuturuza na kuuza maziwa katika mazingira safi.

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupungua kwa ubora wa maziwa na faida ya mauzo.

**VIFAA**

Mabanda ya ndama na ng'ombe wa maziwa

Hori za chakula na maji kwa ajili ya ng'ombe na ndama

Malisho na vyakula bora kwa ndama na ng'ombe wenye mamba na wnaokamuliwa maziwa

Vifaa vya kufanyia usafi nje na ndani ya mabanda ya ng'ombe

Vifaa vya kukamulia, kupimia na kuhifadhi maziwa

**JINSI YA KUFUATA KANUNI ZA UFUGAJI BORA:**

Kuandaa sehemu ya kufugia ng'ombe wa maziwa:

kuna namna nyingi za ujengaji wa mabanda ya kufugia ng'ombe wa maziwa na ndama, kwa kuzingatia idadi ya ng'ombe watakaofugwa.

Itengwe sehemu ya kuzalia ng'ombe , sehemu ya kuishi ndama, sehemu ya kukamulia maziwa na sehemu ya kuishi ng'ombe. Kila sehemu iwe na vifaa vya chakula na maji.

Kuchagua aina bora ya ng'ombe wa maziwa:

Kuna aina nyingi za ng'ombe wa maziwa kwa kuzingatia utoaji wa maziwa mengi. Ng'ombe wa maziwa aina ya genes, jese, eshaya, frishan, na chotara ni bora zaidi kuliko ng'ombe wengine wa maziwa.

**VIGEZO VYA KUMTAMBUA NG'OMBE BORA WA MAZIWA JIKE**

Awe na umbo kubwa la pembe tatu, kiwele kikubwa chenye chuchu nene na ndefu, ametokana na ukoo wa ng'ombe wenye sifa ya kutoa maziwa mengi.

**DUME**

Awe ametokana na ukoo wa ng'ombe wenye kutoa maziwa mengi miguu imara, mwenye uwezo mkubwa wa kupanda majike.

**UTUNZAJI BORA WA NG'OMBE WA MAZIWA**

Kuwapa majani ya kutosha na chakula bora cha ziada.

Kuwapa maji safi na salama ya kutosha kwa ajili na chakula.

Kusafisha mazingira na vyombo vya maji na chakula.

Kutenganisha majike na madume ili wasikae pamoja.

**UPANDISHAJI WA NG'OMBE UNAOFAA**

Ng'ombe jike anapofikia umri wa mwaka mmoja na nusu hadi miwili huwa tayari amefikia umri wa kupandwa na dume. Wakati wa kupandwa ukiwadia ng'ombe jike huonesha dalili zifuatazo:

Wasiwasi, kukimbiakimbia hovyo na kupiga kelele kila mara

Kujaribu kuvunja au kuruka ukuta au uzio wa banda

Kuwapanda majike wenzake na kutulia anapopandwa na majike wenzake.

Sehemu zake zake za uke hutoka ute hutuna na kuwa nyekundu.

**UTUNZAJI BORA WA NG'OMBE MWENYE MIMBA**

Kuwapa majani ya kutosha na chakula kingi cha ziada.

Kuwapa maji ya kutosha ya kunywa ambayo ni safi na salama.

Kusafisha mazingira na vyombo vya maji na chakula.

Kutowahangaisha kwa kuwapeleka huku na huko wala kuwapiga hovyo.

Kuacha kumkamua maziwa ng'ombe mwenye mimba na kumtenga na ng'ombe wengine miezi miwili kabla ya kuzaa.

**UANDAAJI WA SEHEMU YA KUZALIA NG'OMBE**

Kumwandalia ng'ombe mwenye mimba mahali safi pa kuzalia siku moja kabla ya kuzaa

Safisha sehemu uliyoitenga kwa kuzalia ng'ombe halafu tandika nyasi nyingi, kavu na laini sakafuni.

Weka vyombo vya maji na chakula sehemu hiyo na uvijaze chakula na maji ya kutosha.

Mahali hapo pawe na nafasi, hewa na mwanga wa kutosha.

Ng'ombe aingizwe humo anapokaribia kuzaa na aachwe azae mwenyewe. Mara nyingi ng'ombe huzaa mwenyewe bila msaada wowote lakini ukiona anashindwa kuzaa mwite haraka mtaalamu wa mifugo

Mwache ndama akae na mama yake kwa siku nne au tano ili apate kunyonya maziwa ya mwanzo ya mama yake ambayo yana viini lishe vingi na bora kwa afya ya ndama

**UTUNZAJI BORA WA NDAMA**

Kumuondoa kutoka kwa mama yake baada ya siku ya tano na anyweshwe maziwa ya kawaida ya kutosha asubuhi na jioni, bila kupewa majani wala chakula cha ziada kwa wiki tatu.


Kupewa maji safi na salama ya kutosha

Kusafisha mazingira na vyombo vya maji na chakula

Kudhibiti maradhi kwa kuwapa chanjo, matibabu na kunyweshwa dawa ya kudhibiti minyoo

Kupewa majani ya kawaida au kupelekwa malishon wanapofikia umri wa miezi miwili.

Ndama dume kuhasiwa na ndama jike kukatwa chuchu za ziada.



Ndama watengwe na ng'ombe wakubwa kwa miezi mitatu ya mwanzo ili kuwapa matunzo maalumu kwa ajili yao

**NAMNA BORA YA UKAMUAJI WA MAZIWA**

Ng'ombe anayekusudiwa kukamuliwa maziwa aingizwe katika sehemu ya shughuli ya kukamulia maziwa, akiwa amewekewa chakula na maji ya kunywa sehemu hiyo.

Kwa ajili ya usalama, ng'ombe afungwe kamba miguu miwili ya nyuma pamoja ili asipige mateke akamuumiza mkamuaji.

Andaa vyombo na vifaa safi vya kukamulia kama vile kikombe ndoo, deli, vifaa vya kupimia ubora wa maziwa na vitambaa vitatu safi vyeupe kwa ajili ya kusafisha

Maji safi ya vuguvugu yaandaliwe kwa ajili ya kusafishia kiwele na chuchu za ng'ombe kabla ya kukamuliwa maziwa

Mkamuaji maziwa lazima awe msafi na mwenye mavazi anawe mikono vizuri kwa sabuni kabla hajaanza zoezi la ukamuaji maziwa.

**NAMNA SAHIHI YA KUKAMUA CHUCHU ZA NG'OMBE**

Baada ya kufanya usafi unachohitajika, weka ndo ya kukingia maziwa chini ya kiwele cha ng'ombe

Kamata chuchu kwa kiganja cha mkono, uiminyeminye bila kuivuta ukitumia vidole vyote

Maziwa yakitoka kwa kuchuruzika kutoka kila chuchu inayominywaminywa, kinga maziwa kidogo katika kikombe uchunguze kama dalili za kiyungi, damu au vitu visivyokuwa vya kawaida katika maziwa

Ikidhihirika hivyo, ng'ombe huyo ni mgonjwa atengwe na ng'ombe wengine na pata ushauri wa daktari wa mifugo

Ng'ombe mgonjwa akamuliwe mwisho na maziwa yake yasichanganywe na mengine

Ikiwa maziwa ni safi hayana tatizo , mimina maziwa uliyokinga katika kikombe kwenye ndoo ya kukamulia na endelea na zoezi la kukamua maziwa

Baada ya kumaliza kazi ya ukamuaji, pima kiasi cha maziwa kilichopitikana na uyamimine katika vyombo safi vya kuhifadhi kwa kuyachuja kwa kitambaa safi cheupe

Weka kumbukumbu za upatikanaji wa maziwa kwa kila siku na saa yanapokamuliwa katika daftari maalumu la kumbukumbu.

**FAIDA ZA UFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA:**

Hutupatia maziwa kwa ajili ya kunywa na kupikia chai

Humpatia mfugaji fedha kwa kuuza maziwa

Hutupatia mazao ya maziwa kama siagi na jibini

Hutupatia mbolea ya samadi kutokana na kinyesi cha ng'ombe

Hutupatia nyama na ngozi kutokana na kuchinja baadhi ya ng'ombe.

## Maswali

**Andika KWELI kwa sentensi zenye dhana sahihi na SI KWELI kwa sentensi zisizo na dhana sahihi**

Wakati wa kukamuliwa, ng'ombe afungwe miguu ya nyuma pamoja

Chuchu za ng'ombe lazima zisafishwe pamoja baada ya kazi ya ukamuaji kuanza.

Ndama dume huhasiwa na jike hukatwa chuchu za ziada

Baada ya ng'ombe kuzaa ndiyo hukamuliwa maziwa

**Jibu maswali yafuatayo**

Je, ng'ombe anayekamuliwa maziwa hulishwa chakula gain?

Ng'ombe ambaye maziwa yake yana kiyungi hufanywaje?

Baada ya kukamuliwa, maziwa huhifadhiwa kwa namna gain?

Ndama atakaa na mama yake kwa siku ngapi baada ya kuzaliwa?

Dalili zipi zitajulisha jike anataka kupandwa na dume

Aina gani za ng'ombe wa maziwa zinafaa kufugwa katika mazingira ya joto?

# Naipongeza serikali kwa wazo kuwekeza viwanda vya mazao ya mifugo Mwanza

**NISEME** hongera kwa serikali mkoani Mwanza kwa uwekezaji wa viwanda viwili vya kuchakata au kusindika nyama za ng'ombe, mbuzi, kondoo, ambavyo vitaweza kuwanufaisha wafugaji na wananchi wengine wa Mkoa wa Mwanza.

Hatua hiyo siyo haba, inatoa fursa kubwa kwa vijana na wananchi wengine kupata ajira viwandani, lakini imewasaidia wafugaji kuwa na soko la uhakika kwa kuuza mifugo yao katika viwanda hivyo.

Peter Kasele, ni Ofisa Mifugo wa Mkoa Mwanza, aliyefafanua kuwapo viwanda hivyo, kuwa ni moja ya hatua zenye tija mkoani hapa, ikiwa viwanda hivyo vipo katika wilaya za Misungwi na Magu.

Anasema takwimu za idadi ya ng'ombe wa asili katika mkoa mzima ni milioni 1,154,174, ng'ombe wa kisasa wako 5,433, mbuzi wa asili ni 565,570, mbuzi wa kisasa 712 na kondoo wako 133,677.

Hiyo ni kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2019/2020, maana yake ni hadi kufikia sasa 2023, mifugo hiyo itakuwa imeongezeka zaidi idadi yake.

Kutokana na kuwapo idadi kubwa ya watu katika jiji la Mwanza, kwa siku wastani wa ng'ombe 200 huchinjwa katika jiji hili na katika halmashauri zake nane, ni wastani wa ng'ombe100, hata kufanya idadi yake kufikia ng'ombe 300 wanaochinjwa kwa mkoa mzima.

Pia, takwimu hizo zinasema idadi ya mifugo yote inayochinjwa mkoani hubadilika na kuongezeka siku za sikukuu hata kufikia wastani wa 500 kwa mkoa mzima, vilevile mbuzi na kondoo huchinjwa zaidi ya 100 kwa siku, lakini siku za sikukuu hufikia idadi ya 200.

Hivyo, wananchi watafaidika kupata nyama bora kupitia viwandani,kadhalika mifugo aina ya ng'ombe wa asili na kisasa wana faida kubwa ya kupata maziwa.

Kimsingi, serikali bado ina deni la kuhakikisha Mwanza kunajengwa kiwanda cha kutengeneza maziwa, badala ya kuwa na mifugo mingi isiyo na faida.

Tunahitaji wana Mwanza kuiunga mkono serikali kwa juhudi hizo ilizozifanya za kuwekeza viwanda vya nyama katika wilaya hizi, ili kuleta mabadiliko kiuchumi na mapinduzi makubwa ya kuongeza viwanda vingine vya aina hiyo katika mkoa wa Mwanza. Niseme, mifugo hiyo pia ina faida nyinginezo nyingi kama vile ngozi ambazo zinatakiwa kuwa na soko la uhakika, nadhani ingependeza sana kama serikali ingeweza kufikia lengo la kukifufua kiwanda cha ngozi cha zamani kilichokufa 'Mwanza Tanneries'.

Kiwanda hicho kilichopo Ilemela jijini hapa, kinaweza kurahisishia wafugaji na wananchi, pia wafanyabiashara wa zao hilo, kuuza bidhaa hizo kiwandani hapo.

Serikali nayo imekuwa ikitaja kukifufua, lakini inabaki na kitendawili hicho, kinachosubiri kuteguliwa kwa muda mrefu na huenda bado inajipanga au inaendelea kumsaka mwekezaji ambaye hajapatikana.

Kufufuliwa kiwanda hicho, naamini kutaleta mafanikio makubwa na mageuzi ya kiuchumi, ambayo yanatakiwa kuwa ya kisasa zaidi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi zitokanazo na mifugo yetu, katika kutengeneza mabegi, mikanda, viatu, pochi, waleti, mikoba na vitu vingine vingi.

Hapo ndiyo thamani ya zao la ngozi itaongezeka, soko litakuwepo la uhakika na wananchi hususani maskini, watafaidika kununua bidhaa zao za nyumbani kwa bei nafuu, badala ya kununua bidhaa zinazotoka nchi za nje.

Bidhaa nyingi zina gharama kubwa kuzinunua, pia wanazonunua wananchi maskini hazina ubora kudumu utumiaji wake,ikifahamika kuwa viwanda vya ngozi vilivyopo nchini viko mikoa ya Dar-es salaam, Morogoro na Moshi-Kilimanjaro.

Kama serikali itaweza kufufua kiwanda cha 'Mwanza Tanneries' itapunguza makali ya maisha ya wananchi, wanaotumia bidhaa zitokanazo na malighafi za ngozi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kama vile Uganda, Kenya na Bara Ulaya au kwingineko, bei yake ikiwa kubwa na hawezi kuimudu mwananchi wa maisha ya chini, hivyo tunawapongeza serikali kufanya uwekezaji huo mkoani Mwanza.